AFRICAN UNION
الاتحاد الأفريقي
UNION AFRICAINE
UNIÃO AFRICANA
Addis Ababa, Ethiopia, P.O. Box: 3243 Tel.: (251-11) 5513 822 Fax: (251-11) 5519 321
Email: situationroom@africa-union.org

# Tahariri ya pamoja Na Balozi Ramtane Lamamra, Mwakilishi wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya Kunyamazisha Bunduki, na Izumi Nakamitsu, Mwakilishi wa Umoja wa Mafaifa anayeshughulikia Masuala ya Upunguzaji wa Silaha za Vita

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Upunguzaji wa Silaha za Vita
Kutafuta juhudi za kunyamazisha bunduki barani Afrika

Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika (AU), uliofanyika jijini Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 3 hadi 4 Julai 2017, ulitangaza Septemba ya kila mwaka, mpaka 2020, kuwa "Mwezi wa Msamaha Afrika kwa ajili ya kusalimisha na ukusanyaji wa zana ndogondogo za kivita na silaha nyepesi (SALW)." Pia itakuwa inakumbukwa kuwa Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi wa AU uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia 9-10 Februari 2020 ulikubali wazo la mwaka 2020 kuwa wa "Kunyamazisha Bunduki – Kujenga Mazingira Mazuri kwa ajili ya Maendeleo ya Afrika". Kwa hiyo, mwaka 2020 ulikusudia kutoa msisitizo mkubwa kwenye jitihada za viwango vya kitaifa, kikanda na bara katika Kunyamazisha Silaha, na pia kilele cha Mwezi wa Msamaha Afrika.

Hata hivyo, hadi sasa mwaka 2020 umekuwa mwaka wa changamoto za hali ya juu na fursa kwa Afrika katika kusonga mbele kuelekea kwenye amani na maendeleo endelevu kama ilivyo katika Mpango Mkuu wa 2017 wa Hatua za Kiutendaji za Kunyamazisha Bunduki Afrika ifikapo mwaka 2020. Janga la Virusi vya Corona (Covid-19) limeongeza juhudi za nchi wanachama wa AU kwa ajili ya maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii.

Pia limeathiri na kuchelewesha jitihada kwa ajili ya mipango ya kurejesha amani katika bara, kutoka Libya hadi Mali, Bonde la Ziwa Chad na kanda za Sahel ambako msimamo mkali na ugaidi vimeendelea kuwepo bila kupungua. Kufikika kwa maeneo yenye mizozo na migogoro na wadau wa masuala ya kibinadamu kumeathiriwa kwa kiasi kikubwa. Juhudi za kujenga amani na kufikika kwa misaada kwa Nchi Wanachama walioathirika zimepungua. Kwa hiyo, athari mbili za mgogoro na uharibifu uliosababishwa na janga la Covid-19 kwa wale waliopo kwenye hatari kubwa zaidi, yaani wakimbizi, watu waliokimbia makazi yao, wanaorejea na wahamiaji, pamoja na vijana, wanawake, watoto na wazee imezidi kuongezeka.

Kutokana na changamoto hizi, madirisha ya fursa yamefunguka: Mkutano wa 33 wa Wakuu wa Nchi wa AU waliimarisha tena dhamira yao ya pamoja ya kisiasa kwa Nchi Wanachama wa AU kusonga mbele na kunyamazisha bunduki barani. Mkutano ulipendekeza kwamba katika kutekeleza shughuli chini ya dhamira ya mwaka, uangalifu maalum unawekwa na AU, Jumuiya ya Kiuchumi za Kikanda na Utaratibu wa Kikanda kwa ajili ya Uzuiaji, Usimamizi na Utatuzi wa Migogoro na Nchi Wanachama katika masuala / changamoto ngumu za kiusalama, ambayo azimio lake linatarajiwa kutoa gawio zaidi katika juhudi za Afrika za kunyamazisha bunduki na kukuza Afrika isiyo na mizozo.

Mnamo Machi 2020 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU walitoa wito kwa wapiganaji wote kuzingatia usitishaji mapigano katika kipindi chote cha Corona ili kuruhusu ufikiaji wa kibinadamu bila vikwazo katika maeneo ya mizozo na kutoa rasilimali za kushughulikia janga la ulimwengu la COVID-19.

Kutokana na mwendo huo na kujitolea kulikooneshwa kwa ujasiri na Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kupitia Kunyamazisha Bunduki Barani Afrika ifikapo 2020, Jumuiya ya kimataifa, kupitia Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Namba 2457 (2019), limesisitiza umuhimu wa mifumo miwili ya pamoja ya ushirikiano wa Umoja wa Mataifa-AU katika kushawishi mfumo halisi na wa vitendo na kutoa msaada mkubwa kuelekea kuisaidia Afrika kufanya maendeleo yanayoonekana katika kufikia lengo lake la kujenga Afrika isiyo na migogoro. Azimio Namba 2457 (2019), kwa kweli, ni kielelezo cha utayari wa jamii ya kimataifa kuunga mkono utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Umoja wa Afrika wa Hatua za Vitendo za Kunyamazisha Bunduki barani Afrika ifikapo mwaka 2020.

Azimio hilo pia linaunda fursa ambayo inapaswa kutumiwa na Mataifa na vyombo vyote vinavyofanya kazi kwa ajili ya amani na usalama barani Afrika. Hakuna shaka kuwa dhamira endelevu ya kisiasa na rasilimali ni mambo muhimu ya kutafsiri kuwa kweli maono ya Afrika ambayo bunduki zipo kimya, vita ni kitu cha zamani na amani, usalama na maendeleo ya uchumi ni utaratibu wa kisasa.

Ni katika ari kwamba, kwa kuzingatia Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Namba 2457 (2019), Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Upunguzaji wa Silaha za Vita na Tume ya Umoja wa Afrika, na michango ya kifedha kutoka Ujerumani na Japan, wamezindua mradi wa kusaidia shughuli za Mwezi wa Msamaha uliofanywa na Burkina Faso, Cameroun, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Ivory Coast , Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia na Kenya mwaka 2020. Mradi unasaidia nchi hizi katika uhamasishaji na kampeni za uhamasishaji juu ya umiliki haramu wa bunduki na mtiririko haramu wa silaha; ukusanyaji na uharibifu wa zana za kivita ndogo ndogo na silaha nyepesi haramu na risasi zake; na mafunzo ya maafisa wa kutekeleza sheria.

Ingawa inaeleweka kuwa umiliki haramu wa bunduki haramu kwa raia na biashara haramu na ununuzi wa silaha unaofanywa na vikundi vyenye silaha mara nyingi ni dalili ya shida kubwa zaidi ya kiutawala, hatupaswi kuacha kuona ukweli kwamba ni shida kubwa katika juhudi za "Kunyamazisha Bunduki." Njia kamili ya kushughulikia suala hilo kikamilifu inahitaji juhudi endelevu za sehemu zote za jamii. Sio jambo la serikali peke yake. Mashirika ya kijamii na umma wana jukumu la kufanya. Kujumuishwa kwa wahusika hawa katika taasisi za serikali kama vile tume za kitaifa au sehemu kuu za kitaifa za kupambana na mtiririko haramu wa silaha ni pendekezo halali.

Ukiangaliwa kwa upande huu, Mpango Mkuu wa AU kwa ajili ya Hatua za Vitendo za Kunyamazisha Bunduki barani Afrika ifikapo mwaka 2020, pamoja na Mwezi wa Septemba wa Msamaha Afrika vinaunda majibu madhubuti ya kisera kwa Lengo la Maendeleo Endelevu Namba 16.4 ambalo linahimiza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa mtiririko wa silaha haramu ifikapo 2030.

Serikali za Afrika zimejitokeza katika miaka ya hivi karibuni, kiasi fulani kwa kuanzisha tume za kitaifa, kitovu kikuu cha kitaifa na kitovu cha mawasiliano katika serikali zao katika kukabiliana na mtiririko wa silaha haramu. Taasisi hizi ni muhimu katika kufanikisha juhudi za kitaifa zilizoratibiwa kwa utekelezaji wa sera na vyombo vya kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu biashara haramu na usafirishaji haramu wa zana ndogo ndogo za kivita na silaha nyepesi.

Wakati janga la corona limerudisha nyuma baadhi ya juhudi, Umoja wa Mataifa na Tume ya Umoja wa Afrika wameimarisha ushirikiano wao chini ya Sura ya VIII ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, na wataendelea kufanya kazi pamoja kuelekea "Kunyamazisha bunduki" katika bara la Afrika na masuala yanayohusiana na amani na usalama.